https://dspace.org/

Je aka Wa 95 angu Kamati Ya Lua Kuunrwa Ualeta Mabailiko ya Kukiyaika Upya KiSwahili Sanifu?

Karama, Mohamed

2024-12
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/944

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

NI KUFUWATA SAṬI ZA MAJAGINA WA ISIMU

ḌKT. MOHAMEḌ KARAMA, UNIVERSITY OF KABIANGA, KERIČO – KENYA

Je Ṁaka Wa 95 Ṭangu Kʰamati Ya Luğa Kuunrwa Uṭaleta Mabaḍiliko ya Kukiyaṇḍika Upya KiSwahili Sanifu?

Mapisi ya usanifišaji wa kiSwahili yanaoneša kuwa kulikuwa na kauli mbalimbali kuhusu kaďiya hiyo muhimu k̇a luğa yenyewe na elimu k̇a jumla. Yaloṭokeya haḍi tukawa na kiSwahili sanifu kilivo sasa ni maenreleyo ya karne nzima kupunguwa kʰitʰu kiḍogo. Lakini kama wasemavo wanasayansi mabaḍiliko hayana buḍi kuṭokeya na nriyo makuzi. Wanaisimu waṭajika nilowanukuu k̇a piča ṭu wamepambanuwa kuwa kiSwahili (ča wazawa) kina sauṭi zinazosikika waziwazi na zenye umuhimu katika fonolojiya—ṭaaluma ya sauṭi na uwamilifu wake. Kʰamati ya Luğa ilipounra kiSwahili sanifu 1930 “bodirumuni” ilijuwa mfanyiko huu wa kifonolojiya lakini ikapuuza suala hilo na aťari yake k̇a luğa yenyewe; bila kutizamiya kuṭakuwaje k̇enye elimu na teknolojiya. Alhamḍulillahi leo tuna mfumuko wa teknolojiya unaofanya kila kʰitʰu kinukṭaišwe ili kijulikane na watumiyaji wa čočoṭʰe kiličomo uliṁenguni, kefu luğa na maṭamši yake yenye aťari ya kubaḍiliša maana? Hazifayi sauṭi hizo kufanyiwa uṭafiṭi na kuzijumuiša katika kiSwahili sanifu k̇a niya ya k̇ukiṭajiriša kifonolojiya na kisemantiki? Au, ṫenrelee kukiyaṇḍika kiSwahili sanifu ṭafauṭi na kinavoṭamk̇a na ilhali oťografiya yake ni ya sauṭi na viwakiliši vake ni moja k̇a moja? Au, oťografiya ya kiSwahili sanifu ilikomeya 1930? Hatuzingatii mifano ya mabaḍiliko ambapo kila kukiča kuna mtinro mpya wa k̇urejeleya maaṇḍiko k̇enye makala kama humu ni APA Ṭoleo 7. Wanaisimu wasiče k̇a wingi wa sanifu katika kiSwahili kimoja, luğa ni haliya ya kijamii, kama makabila yalivo mengi Afrika Mašariki na yanaiši k̇a uṭangamano, na luğa sanifu kuwa nyingi ni k̇igiza jamii ilivo! Ṫaṭaraji ṁakani 2025 wanaluğa waṭafikiriya zaiḍi kuhusu kʰasi ya teknolojiya na Wekevu Bune zinazoweza kuzitambuwa sauṭi hizi k̇a ukʰeṭʰo. Aiďan, isisahaulike, Kenya kuna Mṭaala wa Utenraji (CBC) ulojaa teknolokjiya mafuṇḍišoni ṁake halafu iwe viṭabu vetu vaaṇḍika na kusema mengine na teknolojiya yasema mengine. InšAllah, Baraza la kiSwahili Kenya (BASWAKE) liṭazawa ṁaka ujawo na ṭʰafiṭi nyingi huku Kenya ziṭariṭibišwa nalo.



In his Roman transcription Taylor notes certain distinctions of sounds. Whether he noted all the differences or not, he at least noted more than any other orthographist of Swahili/Arabic script.

Consonant Symbols used in the Taylor Orthography

	Bi-lab.	*Lab.dent.*	*Dent.*	*Alv.*	*Pal.*	*Velar*	*Glottal*
Stops	p,b		*t*(t)†, *d*(d)	t,d	j(ɟ)	k,g	
			tw				
Asp	p'		*t*'	t'		k'	
Afric.				ch(tʃ)			
Fric.	w(ʋ)‡	v,f		dh,th			
				s, z			
Nasal	m				ny	ng' (ŋ)	
Sem. vow.	w				y		

In Taylor's orthography the *w* and *y* of rhymed syllables are not shown, although these appear in the Swahili/Arabic script. Taylor follows the standard style of having these terminal syllables represented by a vowel, e.g.:

kutua instead of *kutuwa*
ch'iangalia instead of *ch'iangaliya*

Taylor's transliteration of the verse below may illustrate this:

Ai mpewa na pato lipalo mtu kukua;
Angawa mwana mtoto wa kutisha kachewa;

† The symbols in the brackets represent I.P.A. symbols for these sounds.
‡ This is presumed from modern Kimvita.

Piča 1 Čʰimbo: Abdulaziz (1979, uk 76)

Examples:

/p/ paka (smear), paa (roof)

/p^h/ p^haka (a cat), p^haa (a gazelle)

/t/ tembo (beer), tende (elephantitis)
/t^h/ t^hembo (elephant), t^hende (dates)

/ṯ/ ṯupa (throw), ṯini (figs)

/$ṯ^h$/ $ṯ^h$upa (bottle), $ṯ^h$ini (on the floor)

/k/ mkunga (eel), kaa (charcoal)
/k^h/ mk^hunga (mid-wife), k^haa (crab)

/d/ ndoo (bucket)

/ḏ/ nḏoo (come)

Note that the (voiced) implosives - ɓ, ɗ, ɗ̱ and ɠ - have the explosive allophones b, d, ḏ and g respectively, which appear after nonsyllabic nasals in polysyllabic verbs, and after all nasals in monosyllabic verbs:

Examples:

(m̩toto) m̩ɓaya	(kalamu) mbaya
(child) bad	(pen) bad
(mti) m̩ɗogo	(kalamu) ndogo
(tree) small	pen small

Piča 2 Č^{h}imbo: Mazrui (1980, uk 26)

KITIKUU CONSONANTAL SYSTEM

	LABIAL	LABIO-DENTAL	DENTAL	ALVEO-DENTAL	ALVEOLAR	PALATAL	VELAR	GLOTTAL
STOPS	p, b*			t̪, d̪*	d*		k, g*	
FRICATIVES		f, v	θ, ð		s			h
AFRICATES					š, č	ǰ*		
LIQUIDS					l, r			
GLIDES	w					y		
NASALS	m, mb		nð nθ		ndr nd		ŋ, ŋg	

*implosives

Piča 3 Čʰimbo: Bakari (1985, uk 326)



badala ya 'tia', na 'uwa' badala ya 'ua'. Haya yatokana na maandishi ya Kiswahili kwa harufu za Kiswahili/Kiarabu badala ya Kiswahili/Kilatini, na vile vile kwa kuwa harufu zenyewe zimefuata matamshi yenyewe; maana yake Wamvita waitumia *y* na *w* kwa wembamba wakati wa kusema.

Tafauti nyengine kama *'takwenda* (*t* ni ya kupasua menoni) badala ya 'nitakwenda', au *yuwaja* badala ya 'anakuja', *yatungwavyo* badala ya 'yanavyotungwa' na kadhalika. Hapana shaka msomaji atazigundua kila akiyasoma mashairi haya na mengine ya Kimvita.

Ziko tafauti nyengine za matamshi ambazo si dharura sana hapa maana hazikutokea kwa wingi katika mashairi haya. Tafauti zenyewe ni kuwa baada ya *t* kuna harufu nyengine pia ambazo hutamkwa kwa kupasuliwa au kwa unene, na nyengine ambazo hutamkwa kwa wembamba. Mifano ni kama hii:

Chako ina *ch* kavu, na *chicha ch* ya kwanza ni ya kupasua.
Dau ina *d* nene, na *dua* ina *d* nyembamba.
Kaa (keti) ina *k* kavu lakini *kaa* (wa pwani), *k* yake ni ya kupasua.
Ndovu ina *d* nyembamba.
Ndoana ina *d* nene, na mara nyengine hukaribia kuwa *nr* (*nroana*) katika kutamka kwake.
Paa (la nyumba), *p* yake ni kavu, na *paa* (wa mwituni) ina *p* ya kupasua.
S vile vile ina *sw* Kiswahili/Kiarabu kama *swala*, *waswiya*, *swiswi* (sisi), *swi* (samaki).
W inatamkwa baina ya *v* na *w*, yaani *w* yenyewe inatamkwa kwa wembamba.

Katika kitabu hiki, tafauti baina ya Kimvita na 'Ki-Standard' zimeachwa pasi na kuhulutiwa ili ladha ya mashairi haya isifujike, na pia kumzidishia na kumpanulia msomaji mazingira yake ya lugha kwa kumpambanisha na lafudhi ya Kimvita ambayo nayo ina Kiswahili kilichoenea.

Ilimu ya Arudhi ya Kiswahili yazidi kuchunguliwa na, kwa hivyo, yazidi kufahamiwa. Tusiwe na haraka kutafuta aina za mashairi ya kigeni na kuzipachika juu ya ushairi wa Kiswahili, halafu tukadai kuwa hayo ni mashairi ya Kiswahili. Huko ni kama kuvaa nguo inayokupwaya, haikupendezi na kila mmoja aona. Tungo kama hizo 'ha zitamu, ha zinyamu' kama tusemavyo Kimvita.

Kwa wale ambao ndio mwanzo wakilimke Kiswahili, tungo za

22

Piča 4 Č^{h}imbo: Shihabudin (1970, uk 22)

Piča 5 Čʰimbo: Massamba n.w (2004, Jalada)

5 Lau sikuwa wapenḏa hungekaa ukililiya magofu wala hungekosa usingizi kwa kukunbuka *bān* (namna moja ya mti wa kiMisri) na mlima.

6 Wee wakanushaje kuwa wapenḏa na hayo maṯozi yakumiminikayo na kukonda ulikokonda ni mashahiḏi wasokanushika kuwa mahaba yankushika kweli na kweli.

7 Ṯena hilo si ṯuu, huko kukonda na hayo maṯozi yanfanya misṯari miwili katika maṯavu yako, misṯari yenyewe inkaa kama mauwa ya Beḏuini (yaitwayo *bahār* na *'anam*).

8 Naam, n kweli hayo usemayo, na sababu ya balaa hii yoṯ´e, nlimuota nimpenḏae usingizini, na tangu siku hiyo usingizi unnipaa, na hivi ndivyo mahaba yafanyavyo, hukuondoleya raha zoṯ´e yakakuleteya adhabu zoṯ´e.

9 Huko kunilaumu kwa haya mahaba yangu ya kibanii udhera ni kunioneya, lau waṯunga haki hungenilaumu.

10 MNGU asikupe mateso haya yangu, mii maraẓi yangu hayana kupoa, na wadak´u na masabasi waniaziri kila mahali.

11 Wewe kwa hakika wanipenḏeleya wema ndiyo ukanipa naṣaha, lakini mimi si kuwa siisikizi ṯuu hiyo naṣaha yako, bali haṯa kuisikiya siisikii, maana mashikiyo ya mwenye kupenḏa, akilaumiwa huzibika akawa kiziwi.

12 Kama nkusikiza naṣaha, ngesikiza naṣaha ya nvi, maana hizi nvi zilizonijaa kiṯwa tele ni kama zananbiya: 'Ee mṯovu wa haya, wee hujioni ushakuwa mzee, hufai kwendeleya na manbo ya ujana ṯena, wat´u woṯ´e wakuṯeka'. Lakini mimi siṣaḏiki kuwa nshakuwa mzee, naona ati hizi nvi zinkuja ṯuu, najiona mwenyewe nkali kijana, ndiyo kwanza mk´oko waalika mauwa waṯa nṯeze kwanza.

Piča 6 Čʰimbo: Omar (1999, uk 7)



SHEN ṮE: Kushoṯo.

SUN: Ahsanṯa. (*Baaḏa ya muḏa mchache yu-katika kusinzia.*) Huṯaki ṯena wanaume, ee?

SHEN ṮE (*Aṯabasamu.*) Lakini maguu yangu hayana matege.

SUN: Labuḏa.

SHEN ṮE: Si labuḏa.

SUN (*Auṯegemea mkungu kwa machofu alionayo.*) Lakini maaḏamu sijala tangu juzi wala sijanwa tangu jana, siwezi kukupenḏa haṯa nikajaribu.

(*Kimya.*)

SHEN ṮE: Ni uzuri katika mvua.

(*Wong yuaja huku aimba.*)

WONG: Ni hasara kazi yangu kwa mvua ilioko,
Hakuna aṯakae haṯa moja kopo,
Nawauzia wenzangu naja kwenu huko huko.

Hii ni ṯaabu yangu kwa mvua ilioko,
Haṯa muhisani wangu hahiṯaji robo kopo,
Rehema hii ya miungu imenipa sikiṯiko.

Nasema ya sawa jana niliota,
Hakunyi mvua kaṯu kutopiṯa,
Maji muṯanunua nami faiḏa ṯ'apata.

Piča 7 Čʰimbo: Brecht, Shepardson na Marshad (1980, uk 45)

Mayelezo mačače kuhusu piča hizo

Sikuṭaka katika kijumbe hiči k̇eleza sana kuhusu fonolojiya, fonimu, na oťografiya k̇a sababu nišayaeleza haya k̇enye makala yangu, Karama (2022). Ni kukumbuša ṭu na kuweka ṭamaa angaa ṁaka ujawo uwe ṁaka wa kiSwahili sanifu kučanuka ṇčini Kenya na kupata uhayi mpya.

Amma piča hizo zaṭoka k̇enye kazi kʰuu zilofanywa ni wanaisimu na waṭafiṭi waṭajika wa kiSwahili na kiSwahili sanifu k̇a ujumla. Piča 1 mukṭaďa wake ni wakaṭi Marehemu Profesa Mohamed Abdulaziz alipokuwa anafafanuwa maaṇḍiko ya miswada ya Muyaka iliyoandik̇a ni Ṁalimu Taylor k̇a hati za kiRumi na alihifaďi sauṭi zoṭʰe za kiMviṭa, lahaja moja ya kiSwahili. Piča 2 ni uṭafiṭi wa Profesa Alamin Mazrui, Mungu atuwekee, na hapo alikuwa anafafanuwa fonolojiya ya kiMviṭa lakini piya akiyoneša ṭafauṭi za maana k̇a kiSwahili sanifu. Piča 3 ni jeḍwali aliločora Profesa Mohamed Bakari, Mungu atuwekee, k̇a moja ya lahaja ṭisiya alizoziyelezeya mofofonolojiya zake. Kiyambatišo hičo na va lahaja zoṭʰe alizošuğulikiya aliweka sauṭi za kifonetiki zipatikanazo nraniṁe. Piča 4 ni mayelezo ya Šihabuḍin Čirağḍin kuhusu maṭamši ṭafauṭi ṭafauṭi ya kiMviṭa katika mašairi ya Usṭaď Ahmaḍ Nassir. Piča 5 ni jalaḍa la kazi hiyo muhimu ya Marehemu Profesa D.P.B Massamba aloifanya na wenziwe lakini haswa ni hilo jeḍwali alilorejeleya nrani ya kiṭabu hičo na alifafanuwa kuwa ni fonimu za kiSwahili sanifu (uk 41). Marehemu Maalim Yahya alikuwa mṭafiṭi na alifunza kiSwahili SOAS, University of London na aliyaṇḍika kazi kaďaa kuhusu kiSwahili Asiliya mojawapo ni hiyo ṭafsiri ya *Qasiḍa ya Burḍai* k̇enye Piča 6. MaProfesa Abedi Shepardson na Hassan Marshad, Mungu atuwekee, waliṭafsiri kazi ya Bertolt Brecht na kuhifaďi sauṭi za kiSwahili Asiliya (Piča 7); lakini kazi hiyo haiko ṭena madukani wala k̇a mčapišaji. Wanaisimu woṭʰe hawo walivumbuwa ṁaṇḍiko muwafaka kuwakiliša ṭakriban sauṭi zoṭʰe za kiSwahili.

MAREJELEO

Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka: 19th century popular poetry*. Kenya Literature Bureau.

Bakari, M. (1985). *The morphophonology of the Kenyan Swahili Dialects*. Reimer.

Brecht, B., Shepardson, A. na Marshad, H. A. (1980). *Mtu mzuri wa Setzuan*. Kenya Literature Bureau.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Msanjila, Y. P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili sanifu (FOKISA) sekondari na vyuo*. TUKI.

Mazrui, A. M. (1981). *Acceptability in a planned standard: The case of Swahili in Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijačapišwa). Stanford University, Stanford.

Omar, Y. A. (1999). Burdai ya Al Busiri. Katika *AAP*. *60* (1999), 5-20.

Shihabudin, C. (1970). Utangulizi wa mhariri. Katika Ahmad, N. (1971). *Malenga wa Mvita: Diwani ya Ustadh Bhalo*. Oxford University Press.

Kongole: Wa kušukuriwa ni Mola k̇a kutuwezeša kufanya juhudi zetu katika ṁaka huu 2024. Panapo majaaliwa Yake, tuṭaonana ṭena ṁakani 2025.

Kauli Mtakaso: Mayelezo yaliyomo humu ni yangu na si ya UoK wala Idara yetu. K̇a loloṭʰe kuhusu makala haya na/au Elimu k̇a jumla wasiliyana nami mkarama@kabianga.ac.ke .